policy

Machi 2013

# KUPIMA UNYANYAPAA NA UBAGUZI WA VVU MIONGONI WA WAFANYA KAZI WA AFYA

DODOSO FUPI ILIYO SANIFISHWA

Chombo hiki kimeandaliwa na Mradi wa Sera ya Afya (HPP).

Mapendekezo ya chanzo: Health Policy Project. 2013. "Kupima Unyanyapaa na Ubaguzi wa VVU Miongoni Wa Wafanyi Kazi wa Afya: Dodoso Fupi Iliyo Sanifishwa." Washington, DC: Futures Group, Health Policy Project.

Health Policy Project (HPP) ni mradi wa Sera za Afya utakaodumu miaka mitano, ambao umefadhiliwa na Shirika la USAID kupitia mkataba Nambari AID-OAA-A-10-00067, kuanzia September 30, 2010. Mikakati dhidi ya Ukimiwi inasaidiwa na Mpango wa Rais wa Marekani wa Dharura wa Kutoa Usaidizi Kwa Wanaokumbwa na Ukimwi (PEPFAR). Unatekelezwa na Kundi la Futures (Futures Group), ikisaidiana na CEDPA (kitengo cha Plan International USA), Taasisi ya Futures, Washirika Katika Maswala ya Idadi za Watu na Maendeleo Ofisi ya Kanda ya Afrika (PPD ARO), Population Reference Bureau (PRB), RTI International, na White Ribbon Alliance for Safe Motherhood (WRA).

Habari zilizoko katika makala haya siyomaoni rasmi ya Serikali ya U.S na kwa hivyo hayawakilishi maoni ya USAID.

# SHUKURANI

Dodoso hili limeunduwa kutokana na matokeo ya majaribio ya nyajani yaliofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Kufadhili Maendeleo la Marekani ( USAID) Health Policy Project. [1] Hili Dodoso lilijaribiwa katika maeneo sita, yakiwemo: China, Dominika , Misri , Kenya, Puerto Rico, na St Kitts na Nevis . Watafiti wangependa kushukuru wafanyakazi wa vituo vya afya, ambao walichukua muda na jitihada kushiriki katika utafiti huu. Kazi hii haingewezekana bila kuwa na michango bora ya timu za utafiti katika kila eneo. Laura Nyblade (Health Policy Project [ HPP ] na RTI International) aliongoza juhudi za kimataifa, na Aparna Jain ( HPP na RTI International consultant) akitoa usaidizi wa kiufundi. Cynthia Grossman (National Institutes of Mental Health [NIMH]) ilitoa usaidizi katika mchakato wa kuendeleza, kupima, na kulikamilisha dodoso hili. Wapelelezi wakuu, washirika wao, na waliofadhili juhudi za majaribio ya dodoso hili katika kila eneo ni kama ifuatavyo:

China: Li Li (University of California, Los Angeles ) na Jihui Guan (Fujian Provincial Center for Disease Control and Prevention); ufadhili ulipewa na ruzuku kutoka National Institutes of Mental Health (NIMH), (R01MH081778 - 04S1)

Dominika : Roger McLean (University of the West Indies), Marjan De Bruin (University of the West Indies), Julie Frampton (National HIV and AIDS Response Programme, Dominika ) na Wendell Thomas (Caribbean Data Management Systems ); kazi yao ikiwezeshwa na Health Policy Project (HPP), ambao wamefadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimatiaifa (USAID).

Misri: Manal Benkirane (Global Disease Detection and Response Program at the U.S. Naval Medical Research Unit No. 3, Cairo) na Anna- Leena Lohiniva (Global Disease Detection and Response Program at the U.S. Naval Medical Research Unit No. 3, Cairo); wakifadhiliwa na Ford Foundation

Kenya : Janet Turan (University of Alabama, Birmingham) na Zakaria Kwena (Kenya Medical Research Institute) , kwakiwa na msaada kutoka Family AIDS Care and Education Services (FACES), Nyanza Provincial Ministries of Health, na Kenya Medical Research Institute (KEMRI); wakiwezeshwa na HPP

Puerto Rico : Nelson Varas Diaz (University of Puerto Rico) na Francheska Cintron Bou (University of Puerto Rico); walifadhiliwa na ruzuku kutoka National Institutes of Mental Health (NIMH), (1R01MH080694)

St Kitts na Nevis : Roger McLean (University of the West Indies), Marjan De Bruin (University of the West Indies), Gardenia Destang - Richardson (National HIV and AIDS Programme, Saint Kitts and Nevis), Nadine Carty-Caines (National HIV and AIDS Programme, Saint Kitts and Nevis), na Wendell Thomas (Caribbean Data Management Systems ); wakiwezeshwa na HPP.

[1] Health Policy Project. 2012. “Measuring HIV Stigma and Discrimination Among Health Facility Staff: Field-tested Questionnaire.” Washington, DC: Health Policy Project. Available at: www.healthpolicyproject.com.

# UTANGULIZI

***Chombo kipya kilichofanyiwa majaribio kote duniani cha kupima unyanyapaa na ubaguzi unaotoambatana na VVU katika vituo vya afya***

Kwa watu ambao wanaishi na kuadhirika na virusi vya ukimwi (VVU), unyanyapaa na ubaguzi katika vituo vya afya ni kikwazo kikubwa sana kupata huduma za kiafya au kushirikiswa. Watafiti wamenakili mifano mingi kote duniani ambapo watu wanaoishi na VVU wakipokea huduma duni ama kuwekewa vikwazo wasipokee huduma hizi. Hata ingawa maendeleo yamepatikana katika mafunzo na hatua zingine za kupunguza unyanyapaa unaohusiana na VVU katika vituo vya afya, mikakati hii haijaingizwa kuwa desturi na mazoea ya kila siku, au kutekelezwa kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, vyombo vya kupima unyanyapaa vilivyopo ni virefu mno na huchukua muda mwingi vinapotumika, kiwango ambacho havifai kutumika kwenye vituo vya afya.

Katika jitihada za kushughulikia maswala haya, timu ya kimataifa ya watafiti walitengeneza dodoso lililo fupi, na kusanifishua kimataifa kwa ajili ya kupima unyanyapaa na ubaguzi katika vituo vya afya. Chombo hiki kinawezesha ufuatiliaji wa mara kwa mara wa vipimo vya unyanyapaa pamoja na, upanuzi na uboreshaji wa mikakati na miradi inayohusiana na virusi vya ukimwi katika vituo vya afya.

Dodoso hili lilitengenezwa na kujaribiwa kwa njia ya mchakato shirikishi, ukihusisha wataalamu kutoka nchi nyingi. Wataalamu hawa walikubaliana kuzingatia maeneo manne ambayo yanalenga unyanyapaa na ubaguzi katika mazingara ya huduma ya afya, yakiwemo : 1) hofu ya kuambukizwa VVU miongoni mwa wafanyakazi wa vituo vya afya; 2) maonevu na chuki zikielekezwa kwa watu wanaoishi na, au wanaodhaniwa kuishi na VVU; 3 ) unyanyapaa na ubaguzi unaoonekana moja kwa moja na ule unaoelekezwa kwa mtu anayehusiana na mtu anayeishi na VVU, kama daktari anayetibu mgonjwa aneyishi na VVU; na 4) sera na mazingara ya kazi.

Baada ya kuliunda dodoso hili watafiti walilijaribia China ( n = 300), Dominika (n = 335 ), Misri (n = 300), Kenya (n = 350), Puerto Rico (n = 301 ), na St Kitts/Nevis (n = 307 ). Majaribio haya yalihusisha kuuliza maswali wafanyikazi waliohitimu taaluma ya matibabu na wafanyikazi wasio na taaluma ya matibabu, na ilihusisha mchanganyiko wa maswali ya mtu mwenyewe kujijazia na yale ya mhoji kuuliza mhojiwa na kujaza kenye fomu. Baada ya majaribio ya nyanjani, timu ya watafiti walikusanyika tena kujadiliana kuhusu uadilifu wa dodoso hili kwenye maeneo hayo sita ya majaribio; wakizingatia maswala ya vipimo vya kisaikolojia na pia mambo mengine ya kimuktadha.

Dodoso lililotokea linapima vitu vinavyoendeleza unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana VVU wa wafanyikazi wa vituo vya afya vinavyoweza kurekebishua kwa njia ya miradi. Pia dodoso linanasa kushuhudia kwa unyanyapaa na ubaguzi unaotokana na VVU kwenye kituo cha afya; na pia kiwango ambacho wanaotoa huduma za afya wanaelekezewa unyanyapaa na ubaguzi kwa sababu ya kutoa huduma kwa watu wanaoishi na, au wanaaminika kuishi na VVU.

Dodoso mbili zinapatikana kwa umma: toleo fupi, kwa kutathmini miradi, na toleo la kina kwa madhumuni ya utafiti. Kila mojawapo ya dodoso linaweza kutumika kwa ajili ya mazingira ya kiwango cha juu au cha chini cha maambukizi ya VVU.

Habari zaidi kuhusu utekelezaji zitapatikana katika makala ya mwongozo ambayo yatatolewa. Kwa habari zaidi, tafadhali wasiliana na Laura Nyblade kwa anawani ya barua pepe: lnyblade@rti.org

# SEHEMU YA 1: HABARI ZA KIMSINGI

***Kwanza, tutakuuliza juu ya historia.***

1. Ulikuwa na miaka mingapi katika siku yako ya kuzaliwa ya mwisho? ☐ miaka
2. Wewe ni wa jinjia gani?

   ☐ Mwanamke ☐ Mwanaume

3. Kazi yako ni ipi?

| | | |
|---|---|---|
| ☐ Mhasibu | ☐Keshia | ☐ Mtunza usafi |
| ☐ Daktari mzaidizi | ☐Daktari wa meno | ☐ Fundisanifu wa meno /Mtunza usafi wa meno |
| ☐ Daktari | ☐Mfundishaji | ☐ Fundisanifu wa mahabara |
| ☐ Mfanyakazi wa afya ya jamii/Mweliminshaji wa rika | ☐Mhifadhi rekodi | ☐ Fundisanifu wa matibabu |
| ☐ Muuguzi | ☐ Mchanganyaji dawa | ☐ Mpokezaji |
| ☐ Mlinda usalama | ☐ Muhudumu wa chumba cha wagonjwa (wodi) | ☐ Mchukuliwa damu |
| ☐Nyingine: ☐ | | |

4. Katika wiki ya kawaida, ni karibu wagonjwa wangapi wenye virusi vya ukimwi ambao unapatia utunzi au hudumu?

   ☐

5. *Umewahi kupata mafunzo kwa mambo yafuatayo?*: (chagua yote yanayowezekana)
   a. Unyanyapaa na ubaguzi unaotokana na virusi vya ukimwi ☐
   b. Uthibiti wa maambukizo na tahadhari ya kijumla (ikiwemo kumeza dawa baada ya kuwa katika hatari ya maambukizo) ☐
   c. Hali ya mgonjwa kukubali baada ya kupewa habari, faragha na usiri ☐
   d. Unyanyapaa na upaguzi unaotokana na makundi maalumu yalio uhatarishi wa kupata maambukizi ya VVU, ikiwa ni pamoja na wauza ngono, wajidunga, na wanaume wanaojamiana na wanaume wenzao. ☐

# SEHEMU YA 2: UDHIBITI WA MAAMBUKIZI

***Sasa,tutakuuliza juu ya wasi wasi wako kuhusu maambukizi katika kituo chako cha afya.***

6. Utakuwa na wasi wasi kiasi gani ya kupata ukimwi ukiyafanya yafuatayo?

   *[Kama yoyote ya kazi zifuatazo si jukumu lako, (au unaishi na virusi ya ukimwi), tafadhali chagua 'Hainihusu']*

   a. Kushika nguo or matandiko ya mgonjwa anayeishi na virusi vya ukimwi

      ☐ Sina wasi wasi ☐ Wasi wasi kidogo

      ☐ Nina wasi wasi ☐ Nina wasi wasi nyingi

      ☐ Hainihusu

   b. Kufunga vidonda vya mgonjwa anayeishi na virusi vya ukimwi

      ☐ Sina wasi wasi ☐ Wasi wasi kidogo

      ☐ Nina wasi wasi ☐ Nina wasi wasi nyingi

      ☐ Hainihusu

   c. Kutoa damu kwa mgonjwa anayeishi na virusi vya ukimwi

      ☐ Sina wasi wasi ☐ Wasi wasi kidogo

      ☐ Nina wasi wasi ☐ Nina wasi wasi nyingi

      ☐ Hainihusu

   d. Kuchukua joto ya mwili ya mgonjwa anayeishi na virusi vya ukimwi

      ☐ Sina wasi wasi ☐ Wasi wasi kidogo

      ☐ Nina wasi wasi ☐ Nina wasi wasi nyingi

      ☐ Hainihusu

7. Je, kwa kawaida, wewe hutumia hatua yoyote kati ya hizi zifuatazo wakati unapopeana utunzi au huduma kwa mgonjwa anayeishi na virusi vya ukimwi?

   a. Kuepuka kugusana naye

      ☐ Ndio ☐ La ☐Haihusu

   b. Kuvaa mipira ya mikono mara mbili

      ☐ Ndio ☐ La ☐Haihusu

   a. Hatua zozote maalum ambazo huchukua kwa wagonjwa wenya virusi vya ukimwi ambazo huchukua kwa wagonjwa wengine

      ☐ Ndio ☐ La ☐Haihusu

## SEHEMU YA 3: MAZINGIRA YA KITUO CHA AFYA

***Sasa, tutakuuliza juu ya mazoea/desturi katika kituo chako cha afya na ushuhuda wako wa kufanya kazi kwa kituo kinacho tunza watu wanaoishi na virusi vya ukimwi.***

8. Kwa miezi 12 iliyopita, umewahi kumwona mtu anayeishi na virusi ya ukimwi katika kituo chako cha afya?

   ☐ Nidyo → enda swali 11
   ☐ La → ruka mpaka swali 12
   ☐ Sijui → ruka mpaka swali 12

9. *Kwa miezi 12 iliyopita*, ni mara ngapi umeona yafuatayo katika kituo chako cha afya?

   a. Wahudumu wa afya wasiotaka kutunza mtu anayeishi na virusi vya ukimwi.

      ☐ Hakuna kamwe ☐ mara moja au mbili ☐ mara kadhaa ☐ wakati mwingi

   b. Wahudumu wa afya anayetoa huduma wa ubora chini kwa mgonjwa anayeishi au anayefikiri anaishi na virusi vya ukimwi akilinganisha na wagonjwa wengine

      ☐ Hakuna kamwe ☐ mara moja au mbili ☐ mara kadhaa ☐ Wakati mwingi

   c. Wahudumu wa afya wanaoongea vibaya kuhusu watu wanaoishi au wanaodhaniwa kuishi na virusi vya ukimwi

      ☐ Hakuna kamwe ☐ mara moja au mbili ☐ mara kadhaa ☐ wakati mwingi

10. *Kwa miezi 12 iliyopita, ni mara ngapi:*

   a. Umeshuhudia watu wakiongea vibaya juu yako kwa sababu unatunza wagonjwa wanaoishi na virusi vya ukimwi?

      ☐ Hakuna kamwe ☐ mara moja au mbili ☐ mara kadhaa ☐ wakati mwingi

   b. Umetengwa na marafiki na jamii kwa sababu unatunza wagonjwa wanaoishi na virusi vya ukimwi?

      ☐ Hakuna kamwe ☐ mara moja au mbili ☐ mara kadhaa ☐ wakati mwingi

   c. Umetengwa na wafanyikazi wenzako kwa sababu ya kazi yako ya kutunza wagonjwa wanaoishi na virusi vya ukimwi?

      ☐ Hakuna kamwe ☐ mara moja au mbili ☐ mara kadhaa ☐ wakati mwingi

11. Wahudumu wa afya katika kituo hiki cha afya ni wagumu kiasi gani kufanya kazi na mwenzao ikiwa anaishi na virusi vya ukimwi, bila kujali kazi wanazofanya?

   ☐ Sio wagumu ☐ Wagumu kidogo ☐ Wagumu kiasi ☐ Wagumu san

## SEHEMU YA 4: SERA ZA KITUO CHA AFYA AND MAZINGIRA YA

***Sasa tutakuuliza juu ya sera za taasisi na mazingira ya kikazi katika kituo chako.***

12. Katika kituo changu cha afya haikubaliki kupima mgonjwa virusi vya ukimwi bila yeye mwenyewe kujua.

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

13. Nitajipata taabani kazini nikipagua wagonjwa waliona virusi vya ukimwi.

    ☐ Ndio ☐ La ☐ Sijui

14. Je, unakubali kabisa, kubali, haukubali or haukubali kabisa na kauli zifuatazo?

    a. Kuna vifaa vya kutosha katika kituo changu cha afya ambvyo vinapunguza nafasi yangu kuambukizwa virusi vya ukimwi

       ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

    b. Kuna taratibu/maagizo yaliyosanifishwa katika kituo changu cha afya yanayopunguza nafasi yangu kuambukizwa virusi vya ukimwi

       ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

15. Kituo changu cha afya kina maagizo yaliyoandikwa chini kuwalinda wagonjwa waliona virusi vya ukimwi dhidi ya kupaguliwa.

    ☐ Ndio ☐ La ☐ Sijui

# SEHEMU YA 5: MAONI KUHUSU WATU WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI.

***Sasa tutakuuliza maswali juu ya maoni yako kuhusu watu wanaoishi na virusi vya ukimwi***

16. Je, unakubali kabisa, kubabi, haukubali or haukubali kabisa na kauli zifuatazo:

    a. Watu wengi wanaoishi na virusi vya ukimwi hawajali hata kama wanaambukiza watu wengine.

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

    b. Watu wanaoishi na virusi vya ukimwi wafaa waone aibu wenyewe.

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

    c. Watu wengi wenye virusi vya ukimwi wako na wapenzi wengi

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

    d. Watu wanaambukizwa na virusi vya ukimwi kwa sababu wanajiingiza kwa tabia zisizofaa

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

    e. Virusi vya ukimwi ni adhabu ya tabia mbaya.

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

17. Wanawake wanaoishi na virusi vya ukimwi wanafaa wakubaliwe kupata watoto ikiwa wanataka.

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

18. Tafadhali tuambie kama unakubali kabisa, unakubali, haukubali or haukubali kabisa na kauli ifuatayo:

    a. Kama ningekuwa na uamuzi , ningelipenda nisitume hudumu kwa watu wanaojidunga madawa za kulevya.

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

    b. Kama ningekuwa na uamuzi, ningelipenda nisitume hudumu kwa wanaume wanaojamiana na wanaume wenzao.

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

    c. Kama ningekuwa na uamuzi, ningelipenda nisitume hudumu kwa wauza ngono (fafanua: mwaume au mwanamke au wote wawili kulingana na mkutadha).

    ☐ Kubali kabisa ☐ Kubali ☐ Haukubali ☐ Haukubali kabisa

HEALTH POLICY PROJECT
www.healthpolicyproject.com

1331 Pennsylvania Avenue NW, Suite 600
Washington, DC 20004
policyinfo@futuresgroup.com